

---

*the **M**pingo **C**onservation **P**roject*

---



---

**MCP Misitu ya Jamii Tanzania**  
**Uthibitishaji wa Pamoja**

---

*SD07 Taratibu za uvunaji Mbao*

Toleo la 1.0 – 02/02/10

---

# Yaliyomo

---

<b>UTANGULIZI .....</b>	<b>3</b>
<b>MAJUKUMU YA MSIMAMIZI WA UVUNAJI.....</b>	<b>4</b>
<b>TARATIBU ZA UVUNAJI .....</b>	<b>5</b>
<b>VIFAA VYA UVUNAJI .....</b>	<b>6</b>
Vifaa vya kujikinga na athari.....	6
Matumizi ya vifaa vya uvunaji .....	6
<b>MAFUNZO .....</b>	<b>7</b>
<b>USIMAMIZI WA ENEO LA UVUNAJI.....</b>	<b>8</b>
Kupunguza mabaki .....	8
<b>USAFIRISHAJI NA UTOAJI WA MAGOGO .....</b>	<b>9</b>

---

## Utangulizi

Uvunaji magogo ni mojawapo ya shughuli za hatari sana. Vyanzo vikuu vya athari katika uvunaji ni ukosefu wa mafunzo, mbinu duni za uvunaji na kutokuwepo kwa hatua za kiusalama za uvunaji magogo.

Kutokana na athari zilizopo katika uangushaji miti, urengetuaji, upakiaji na upakuaji magogo ni muhimu kuchukua hatua za tahadhari juu afya, usalama na masuala ya mazingira.

Sababu za kuwa na viwango salama vya uvunaji.

- Kupunguza gharama na madhara yanayoweza kupunguza ufanisi kutokana na majeraha na magonjwa.
- Kupunguza majeraha na magonjwa katika shughuli za uvunaji mazao ya misitu.
- Kujenga mahusiano mazuri kati ya wakataji na wafanyabiashara wa mazao ya misitu.
- Kujenga taratibu za usalama ambazo zitatoa mwongozo katika kubadilisha mtizamo, mwenendo, utendaji kazi na kuleta desturi/utamaduni mpya wa ufanyaji kazi kiusalama.
- Kutimiza na kuendana sawa na matakwa ya uthibitishaji misitu ya FSC ili kutoa motisha na tija kwa wafanyabiashara ya mazao ya misitu ambao wanafuata taratibu na viwango vya uvunaji salama.
- Kuongeza kipato kwa kila gogo kwa kupunguza mabaki/uchafu utokanao na uvunaji.

Kwa ujumla mafunzo bora, mipango mizuri, mbinu bora za uvunaji, usalama na kutumia akili katika kazi sio tu huleta usalama kazini bali huongeza pia ubora wa gogo lililokatwa.

## Majukumu ya Msimamizi wa uvunaji

1. Msimamizi wa uvunaji ni **LAZIMA** awe kiongozi katika shughuli nzima ya uvunaji na atawale zoezi zima kwa kujua **majukumu** yake na **kuyafuata**. (Lazima awe mkali na asiyetaka mzaha)
2. Msimamizi ni lazima ateleze viwango vya Usalama na ufanisi katika uvunaji misitu ambavyo vimewekwa na Umoja wa uthibitishaji kwa kutumia vyombo salama na vinavyotakiwa katika shughuli za uvunaji.
3. Ni sharti msimamizi kuhakikisha kuwa wakataji wanao uelewa juu ya viwango vya usalama na ufanisi kazini, taratibu na mahitaji ya kazi na lazima ajiridhishe kuwa maelekezo yameeleweka vyema kabla ya kuanza ukataji.
4. Ni lazima ahakikishe kuwa vifaa na vitendea kazi viko katika hali nzuri na vinatumika vyema. (mfano vyombo vya kukatia vimenolewa)
5. Msimamizi ni lazima ahakikishe kuwa kazi imepangwa vizuri na inafanyika kwa kupunguza athari za ajali kazini na mazingira ambazo yanaweza yakasababisha madhara kwa wakataji au afya zao.
6. Msimamizi ni lazima atathimini mahitaji ya maelekezo au mafunzo ya ziada, au elimu zaidi kwa wakataji kulingana na matakwa ya viwango vya salama na ufanisi katika uvunaji wa misitu.
7. Endapo msimamizi atagundua ukiukwaji wa viwango vya usalama na ufanisi katika uvunaji misitu ambao umefanywa na mkataji, ni lazima achukue hatua mara moja na kutoa amri. Hatua atakazochukua ni kama kumwamuru mkataji nini cha kufanya, kumwamrisha kuvaa na kutumia vitendea kazi, kusimama mbali na eneo la ukataji au kutoa onyo kali. Kama hatua hizo hazitazaa matunda, tatizo ni lazima lipelekwe mbele kwa Meneja wa Umoja.
8. Msimamizi ni lazima ahakikishe yafuatayo;
  - (a) Ni lazima ajaze Fomu ya vigezo vya Uvunaji Salama wa misitu (Fomu SF 08) ili kuendana na Viwango vya usalama na ufanisi vya uvunaji misitu vilivyowekwa.
  - (b) Kuzingatia daima mbinu salama za utendaji.
  - (c) Matumizi bora ya vitendea kazi vya kujikinga na athari mbalimbali.
  - (d) Matumizi bora ya vifaa vya uvunaji.
  - (e) Sanduku la Huduma ya Kwanza linakuwepo wakati wa uvunaji

### *Namna ya kuwa Msimamizi wa uvunaji*

Ili kufuzu kama msimamizi wa uvunaji, mtu anatakiwa kuwa amepitia mafunzo ya; an Approved Logging Supervisor, someone must have been trained in:

- Taratibu za uangushaji mti katika mwelekeo salama kama ilivyobainiwa katika kabrasha hili.
- Namna ya kutumia vyombo vya uvunaji na jinsi ya kunoa misumeno
- Huduma ya Kwanza
- Jaribio la namna ya kusimamia uvunaji

Mwisho wa mafunzo haya yote ni kupima uwezo wa msimamizi jinsi anavyoweza kubaini mapungufu na kuchukua tahadhari wakati wa uvunaji.

## Taratibu za uvunaji

Ufanisi katika ukataji miti utafanikiwa tu kwa kufuata njia bora za uvunaji. Ili kupunguza mabaki, matukio ya ajali, kuzuia kupasuka kwa magogo wakati wa kuangusha, vigezo au mambo mbalimbali ni lazima yazingatiwe kabla ya kuangusha mti. Hatua za kufuata wakati wa uvunaji ni:

1. Shughuli zote za uvunaji misitu ni **LAZIMA** zisimamiwe na msimamizi wa uvunaji aliyepatiwa mafunzo na kuidhinishwa.
2. Fomu Na. SF 08 ya vigezo vya uvunaji salama wa misitu ni lazima ijazwe na msimamizi wa uvunaji na ahakikishe kuwa vigezo vyote vimetimizwa (kama kigezo mojawapo hakikufuatwa uvunaji hauruhusiwi kufanyika).
3. Vitendea kazi vyote ni lazima vikaguliwe kuhakikisha viko katika hali nzuri kabla ya kuanza kazi.
4. Mwelekeo wa kuangushia mti kama ambavyo imeelezwa hapo chini ni lazima ufuatwe wakati wote uvunaji unapofanyika katika misitu iliyothibitishwa na ni lazima mwelekeo uamuliwe kabla ya kuanza kukata kwa kuzingatia mwelekeo na nguvu ya upepo, mti ulikoinamia, muonekano wa mti na miti inayozunguka eneo hilo.
5. Kama upepo unavuma sana na kwa nguvu na kuathiri mwelekeo salama wa kuangushia, uvunaji hautafanyika.
6. Mwonekano wa mti ni lazima uzingatiwe kabla ya kukata, mti utaangaliwa kama umepinda, kama umeoza, kama umekufa na matawi yake yakoje.
7. Ni lazima watu wasiohusika na ukataji wakae umbali wa urefu wa mti mara mbili toka mti unaoangushwa.
8. Athari ambazo zinaweza kusababishwa na miti iliyokaribu na eneo la ukataji ni sharti ziangaliwe na kuchukua taadhari.
9. Ni sharti njia ya dharura ya kukimbilia/kujiokoa iandaliwe kabla ya kuanza kukata na iwe nyuzi 45 mkabala na mwelekeo wa kuangushia. Kila mkataji atumie njia yake wakati wa kujiokoa. Pia njia ya kujiokoa ya msimamizi lazima iwe nyuzi 90 kutoka mwelekeo wa kuangushia
10. Wakataji ni lazima wahakikisha wanakaa vizuri bila kuyumbayumba wanapofanya kazi.
11. Eneo la kuweka vifaa vya kazi ni lazima lijulikane kabla ya kuangusha na liwe upande wa kulia au kushoto na vifaa vionekane vyema ili kuzuia wakataji kuvikanyaga wakati wa dharura wanapojiokoa na athari.
12. Eneo kuzunguka mti ni lazima lisafishwe (mafukutu na mawe lazima yaondolewe kabla ya kuanza kukata).
13. Mkato mkuu wa kuangushia/mkato nyuma ni lazima uwekwe katika mwelekeo wa kuangushia na mkato wa chini uwekwe katika upande wa pili.
14. Mkato wa nochi utatumika pale ambapo utahitajika na utakuwa chini zaidi katika shina la mti kutegemeana na mti ulivyo.
15. Mti hautakatwa moja kwa moja, sehemu ya kutosha itaachwa kati ya mkato wa chini na mkato wa kuangushia. Hii inasaidia kuzuia mti kuruka nyuma unapoanguka na kusaidia katika mwelekeo wa kuangushia.
16. Tindo zitatumika inapobidi ili kusaidia mwelekeo wa kuangushaji. Ni lazima tindo iwe karibu na wakataji ili iwe rahisi kuitumia inapohitajika.
17. Msimamizi wa uvunaji ni lazima atoe ishara ya sauti kubwa wakati mti unapoanza kuanguka.
18. Wakati wa kurengeta wakataji wasimame upande wa pili wa gogo.

## Vifaa vya uvunaji

### Vifaa vya kujikinga na athari

Vifaa vya kujikinga na athari vitatolewa ili kutumiwa na wakataji wote. Vifaa hivyo ni magambuti, kofia za ngumu za kukinga kichwa, vifaa vya kuziba pua na gloves za mikononi.

- Msimamizi wa uvunaji ni lazima ahakikishe kuwa vifaa vyote vya kujikinga na athari vimevaliwa kama inavyotakiwa.
- Watu ambao hatavaa vitendea kazi vya usalama hawataruhusiwa kuingia katika eneo la uvunaji kuzunguka mti unaoangushwa.

### Matumizi ya vifaa vya uvunaji

Vifaa vya kukatia wakati wa uvunaji ni msumeno wa watu wawili kwa ajili ya kuangushia na kurengeta, mashoka, mapanga na mashoka na nyundo. Vifaa vingine vinavyotumika wakati wa uvunaji ni kama tupa na tindo.

1. Mashine za kukatia (Chain saws) hazitaruhusiwa katika cheti cha pamoja.
2. Vifaa vyote vitumike kwa kazi iliyokusudiwa tu
3. Kila kifaa ni lazima kikaguliwe na msimamizi wa uvunaji na kama kuna tatizo lirekebishwe kabla ya uvunaji kuanza.
4. Vifaa vyote ni lazima vinolewe vyema
5. Vichwa vya nyundo na tindo ni lazima viwekwe katika hali ya usalama zaidi wakati vinapoanza kuchoka
6. Tupa ni lazima ziwekwe mkono wa kushikia.
7. Vifaa vyote ni lazima viwekwe katika hali ya usalama wakati wa utunzaji stoo, kuvisafirisha na wakati havitumiki ili kuzuia madhara.
8. Vipande vya chuma vinavyotoka kutokana na kutumika kwa chombo ni sharti viondolewe na chombo kisafishwe.
9. Mkono wa shoka ni lazima ushikane sawa na shoka lenyewe.
10. Vishikio vya vifaa ni lazima viwe safi na visiwe na mipasuko.
11. Misumeno yote ni sharti inolewe vizuri na Msimamizi wa uvunaji au mtu yeyote ambaye ni mzoefu kabla ya kutumika..
12. Wakati wa kutumia misumeno itumike ikiwa imenyooka bila kuipinda na ivutwe pasipo kuisukuma.

## Mafunzo

Katika kazi yeyote kama ya uvunaji miti ambayo adhari au ajali hutokea, mafunzo kwa wanaofanya kazi msituni ni muhimu sana.

1. Mafunzo yatatolewa kwa wote wanaofana kazi msituni, mafunzo yatajumuisha pia matumizi bora ya vifaa.
2. Mafunzo kwa wakataji yatafanyika kabla ya kuanza kwa msimu wa uvunaji na mara kwa mara.
3. Taarifa zote za mafunzo na makabrasha ya mafunzo yatatunzwa ili kutunza kumbukumbu. Vyeti vitatolewa kwa wote walioshirikishi mafunzo.
4. Mafunzo yatafanyika kwa nadharia darasani na kufuatiwa na mafunzo kwa vitendo msituni.
5. Mafunzo yatatolewa na mtaalam toka Mradi wa Kuhifadhi Mpingo au sehemu nyingine.
6. Wasimamizi wa uvunaji watapewa mafunzo ya jinsi ya kutumia vifaa vya uvunaji na namna ya kuvifanyia matengenezo kama vile kunoa. Mafunzo ya jinsi ya kunoa na kupanga meno ya misumeno yatatolewa na mtalaam ambaye ni mzoefu.

Rejea katika kipengele cha juu cha majukumu ya msimamizi wa uvunaji kwa maelezo zaidi juu ya sifa zinazotakiwa kwa mtu kuwa msimamizi wa uvunaji.





## Usafirishaji na utoaji wa Magogo

Malori na matekta yatumika kutoa magogo msituni. Hata hivyo, utengenezaji wa barabara mpya ndani ya misitu ya cheti cha pamoja utategemea tathmini ya athari za kimazingira. Hivyo basi matumizi ya malori na matekta utategemea uoto wa asili uliopo na hali ya ardhi husika. Ukataji wa mafukutu na miti midogo utaruhusiwa tu ili mradi miti mikubwa haiangushwi na eneo ambalo mafukutu yameondolewa ni dogo. Ukataji zaidi wa uoto wa asili zaidi ya unene wa sentimita 10 katika kimo cha kifua utahesabika kama utengenezaji wa barabara.

Ni marufuku kuendesha gari au trekta kwa kufuata au kwa kukatisha chanzo cha maji isipokuwa kama kuna njia inayotumika, magari hayo yatumika wakati wa kiangazi tu. Magari ni lazima yakwepe kupita katika maeneo muhimu ya kimila. Utoaji wa magogo hauruhusiwi endapo udongo una unyevu sana.

Kutokana na vikwazo hivyo, magari na matekta lazima yapite karibu zaidi na eneo la uvunaji. Kutoka eneo la uvunaji hadi kwenye gari au trekta, magogo yanaweza kubebwa kwa mkono. Ubebaji wa magogo kupeleka kwene magari ni lazima ufuata njia ambayo haiathiri sana uoto wa asili na kingo za vyanzo vya maji.

### *Uhakiki*

Mwongo huu juu unatokana na maoni ya kitalaam kwamba athari zinazotokana na kusafisha eneo kwa ajili ya njia ya mpya ya magari zinazidi athari za kutumia njia inayotumika ambapo maji hutiririka. Pia kuna changamoto kuwa pale ambapo njia inapita kuelekea mwinuko au chini ya mwinuko inaweza kuwa chanzo cha maji baada ya kusafishwa. Hii ni kusema kwamba si rahisi kuanzisha njia ambayo baadae itakuwa mkondo wa maji.